




KISURA

ALMANUSURA...



UTANGULIZI

Kitabu hiki cha simulizi ya binti Kisura kimeandaliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na World Vision Tanzania, kupitia kampeni ya “Mapambano Dhidi ya Ndoa za Utotoni ni Jukumu Letu Sote”.

Lengo la Simulizi hii ni kuelimisha watoto, vijana na wanajamii kwa ujumla juu ya madhara ya ndoa.za utotoni katika ustawi wa mtoto na wajibu wa mzazi/mlezi katika kumlea na kumlinda mtoto.

Tafiti mbalimbali zinaonesha watoto wengi wanafanyiwa vitendo vya kikatili na unyanyaswaji ikiwemo kuoreshwa katika umri mdogo na hivyo kusababisha kushindwa kufurahia utoto wao na kuwaletea madhara makubwa kiakili, kihisia na kimwili.


Hali hii isipokomeshwa itaendeleza mzunguko wa umaskini na ukatili katika jamii zetu. Tunaamini kuwa kitabu hiki kitachangia katika kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya ulinzi wa mtoto na kuchangia katika kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.



.....
Dkt. John K. Jingu

Katibu Mkuu,

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
(Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)



.....
Gilbert Kamanga

Mkurugenzi Mkuu,

World Vision Tanzania

Wahusika



Baba Kisura



Kisura



Mama Kisura



Mwalimu




Afisa Maendeleo ya Jamii



Afisa Ustawi wa Jamii

MUDA WA JIONI BABA ANAMUITA MAMA...





KISURA AKIJIANDAA KWENDA SHULE




BAADA YA MWEZI MMOJA
UTAOLEWA SABABU UMEKUA NA
HATUNA PESA ZA KUKUENDELEZA



MAMA
NIOLEWE..!

NDIO



WEWE NENDA SHULE
TUTAONGEA VIZURI
UKIRUDI JIONI

KISURA ANAENDA SHULE
AKIWA NA MAWAZO TELE




AKIWA SHULENI ANAONEKANA MWENYE
HUZUNI, MARAFIKI ZAKE WANAMUULIZA



RAFIKI WA KISURA ANASEMA...

UNAKUMBUKA MWALIMU
ALITUFUNDISHA MADHARA
YA NDOA ZA UTOTONI NA
SEHEMU ZA KURIPOTI?



HUKU NYUMBANI; MAMA KISURA NAE ANAONDOKA KWENDA KUCHOTA MAJI KISIMANI



ANAKUTANA NA AKINA MAMA WENZAKE, ANAWAELEZA ALICHOPANGA NA MUME WAKE KUHUSU MWANAE KISURA...




MAMA MMOJA ANASEMA...






NI KWELI TUNAKUMBUKA, NA KUNA
WATU WANAOTOA TAARIFA KWA SIRI
KWA HIYO MAMA KISURA... ANGALIENI
SANA MAAMUZI YENU SIO MAZURI



KWA HIYO
M NANISHAURI
VIPI?







MWALIMU BAADA YA KUSIKILIZA ANAMPIGIA SIMU AFISA MAENDELEO YA JAMII...



HALOO..!
UNAONGEA NA
MWALIMU

NDIO
MWALIMU
SEMA...




KUNA
BINTI HAPA
SHULE WAZAZI
WAKE WANATAKA
KUMUOZA...




ASANTE KWA TAARIFA
NITAWASILIANA SASA
HIVI NA AFISA USTAWI
WA JAMII ILI
TUAMBATANE
NAE...


TUNAWASUBIRI AFISA MAENDELEO
NA AFISA USTAWI WA JAMII WANAKUJA



SAWA
MWALIMU

HAIKUCHUKUA MUDA MREFU AFISA USTAWI WA
JAMII NA AFISA MAENDELEO YA JAMII WAKAWASILILI






MAMA KISURA ALIPOWAONA
TU AKAHISI KUNA JAMBO..



BABA KISURA NAYE AKAPATA HOFU






MAZUNGUMZO YAKAANZA...



MBONA
MMESHAPOKEA
MAHARI? JE, MNAFAHAMU
MADHARA YA MIMBA NA
NDOA ZA UTOTONI?


KUSEMA KWELI TUMESHAPOKEA
MAHARI NA MILA ZETU
ZINARUHUSU KWA SABABU
HAKUNA MADHARA YOYOTE.



HALAFU PESA
ZA KUMSOMESHA
HATUNA




NDOA NA MIMBA ZA UTOTONI
ZINA MADHARA MAKUBWA KAMA
KUHATARISHA MAISHA WAKATI
WA KUJIFUNGUWA...




LAKINI PIA
HUENDELEZA
UMASIKINI NA
UTEGEMEZI


HALAFU MTAKUWA
MNAMNYIMA HUYU
BINTI HAKI YAKE YA
KUPATA ELIMU



KWANI ELIMU INAFAIDA GANI?
ATAPOTEZA TU MUDA...



ELIMU INAMSAIDIA MTOTO WA
KIKE KUJUA HAKI NA WAJIBU
WAKE, KUJIAMINI NA KUFANYA
MAAMUZI SAHIHI...



ATAWEZA KUPATA AJIRA,
KUJITENDELEZA, KUJITEGEMEA
NA KUSHIRIKI KIKAMILIFU
KWENYE SHUGHULI ZA
MAENDELEO






KIUJUMLA ATAWEZA KUJENGA
FAMILIA YENYE MAISHA BORA
KIAFYA NA KIELIMU HIVYO
KUPUNGUZA UMASIKINI




AISEE
KUMBE?

MUME WANGU
KWELI UTAWENZA
KWA HALI YETU
YA UCHUMI?




HIZO NDIZO BAADHI YA
FAIDA NYINGI ZA
KUMSOMESHA MTOTO



CHA MSINGI MFANYE KAZI
KWA BIDII NA MJIUNGE KWENYE
VIKUNDI VYA MAENDELEO ILI
MUWEZE KUPATA KIPATO CHA
KUMSOMESHA KISURA




NAKUKARIBISHA AFISA USTAWI
UZUNGUMZE KUHUDU SHERIA
NA ADHABU KUHUDSANA NA HILI



ASANTE SANA...
KWA MUJIBU WA MABADILIKO YA
SHERIA YA ELIMU YA MWAKA 2016,
MTU YEYOTE ATAKAYE MUOA AU
KUOLEWA NA MTOTO WA SHULE
ATAFUNGWA MIKA THLATHINI
GEREZANI





PIA, MTU YEYOTE ATAKAYEMPA
MTOTO UJAUZITO ATAFUNGWA
GEREZANI MIKA THELATHINI



AIDHA, MTU YEYOTE ATAKAYEHUSIKA
KUMUOZESHA AU KUMUOZA MTOTO
WA SHULE ATAFUNGWA KIFUNGO
CHA MIKA MITANO AU KULIPA
FAINI YA SHILINGI MILLIONI TANO AU
VYOTE KWA PAMOJA








TUMEWAELEWA VIZURI..
HATUTAMWOZESHA BINTI
YETU. BADALA YAKE
TUTAMSAIDIA...



ASANTENI
KWA ELIMU
MLIYOTUPA



HUZUNI IKATOWEKA, FURAHA
IKAREJEA KWA KISURA...



WAGENI WANAONDOKA




ILIBAKI KIDOGO TU
KUKATISHA NDOTO
ZA BINTI YETU NA SISI
KUISHIA GEREZANI



WAHUSIKA/SEHEMU ZA KUTOA TAARIFA



- Ofisi ya Kijiji (Mwenyekiti na Afisa)
- Mjumbe kamati ya ulinzi
- Afisa Maendeleo ya Jamii/Afisa Ustawi wa Jamii
- Polisi: Dawati la jinsia na watoto
- Kituo cha Afya/ Zahanati
- Mashirika yanayotetea haki za watoto
- Shirika linalotoa msaada wa Kisheria
- Shuleni (Mwalimu)



PIGA NAMBA 116 NI BURE

HITIMISHO

Mambo muhimu ya kukumbuka

- Kila mtu anawajibu wa kumlinda mtoto dhidi ya ukatili
- Mtoto ana haki ya kulindwa, kushirikishwa, kuendelezwa , kuishi na kutobaguliwa
- Mtoto ana wajibu wa kutimiza katika ngazi ya familia, shule na jamii
- Toa taarifa haraka sehemu husika pale unapona au kusikia mpango wa ukatili kwa mtoto



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
Chuo Kikuu cha Dodoma,
Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Maendeleo ya Jamii
Jengo Namba 1
S.L P 573
40478 DODOMA
Simu: 255-26-2963341/2963342/2963346
Nukushi 255-26-2963348
Barua Pepe:ps@communitydevelopment.go.tz
Tovuti:www.mcdgc.go.tz

Head Office

World Vision Tanzania (WVT)
Radio Tanzania Road, Off-Njiro Road,
Block C, Plot No. 181 Njiro,
P.O.Box 6070, Arusha, Tanzania
Tel: +255-27 254-9252/253/254
Fax: +255-27-254-9259
Email: tanzania@wvi.org
Website: www.wvi.org/tanzania

Kijarida hiki kimetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na World Vision Tanzania. Haki zote zimehifadhiwa